



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA



Taarifa namba: 045

15/10/2022

TAARIFA KWA UMMA

**TAARIFA YA KUFUNGULIWA KWA STENDI KUU YA MABASI TUNDUMA
ILIOPO KATA YA MPEMBA**

Halmashauri ya Mji Tunduma inapenda kuwataarifu wananchi wote wa ndani na nje ya Tanzania kuwa **Stendi Kuu ya Mabasi Tunduma** iliyopo Kata ya Mpemba Barabara ya kuu ya Kwenda Ileje/Malawi imefunguliwa rasmi kuanzia tarehe 13/10/2022

Hivyo kuanzia sasa Mabasi yote yanayokuja Tunduma kwa Kutumia barabara ya TANZAM yatokayo **Mikoa ya Mbeya, Njombe, Iringa, Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam yataishia stendi kuu ya Mabasi ya Tunduma** iliyopo kata ya Mpemba. Kwa mabasi yanayo elekea/kutoka mkoa wa Rukwa na Katavi yatashusha **kituo cha Mpakani mwa Chipaka (Nkangamo) na Stendi kuu tu**, hairuhusiwi kushusha au kupakia katika vituo vingine vya ndani ya Mji.

Hivyo kama wewe ni mgeni basi utapanda daladala kuelekea Mjini au sehemu nyingine unazotaka kwenda ndani ya Halmashauri ya Mji Tunduma

Kwa wanaotaka kuja zilipo Ofisi za Halmashauri ya Mji, **ukishuka Stendi kuu Panda daladala shuka kituo kinaitwa Chapwa** hapo utapanda Pikipiki au kutembea kuelekea Ofisi ilipo ni umbali wa Kilometa Moja toka kituo cha Chapwa kilipo

Karibuni sana wageni wote Halmashauri ya Mji Tunduma

William Maganga

WILLIAM MAGANGA

**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
HALMASHAURI YA MJI-TUNDUMA**